

TAARIFA YA VIKUNDI VYA KIJAMII NA VICOBA KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA LUSHOTO

1.0 UTANGULIZI

Halmashauri ya wilaya Lushoto ina jumla ya vikundi vya kijamii vilivyosajiliwa ngazi ya Halmashauri 714 kati ya vikundi hivi vikundi 471 ni vikundi vya kuweka na kukopa (VICOBA). Vikundi hivi vinajishughulisha na shughuli mbalimbali za uzalishaji kama vile ufugaji, kilimo, usindikaji, maduka ya rejareja, ufyatuaji wa matofari, miradi ya kuhifadhi mazingira na ujasiriamali. Vikundi vingine vinajishughulisha na utengenezaji wa bidhaa mbalimbali za viwandani kama vile sabuni za maji, sabuni za miche na shampoo.

2.0 UWEZESHWAJI WA VIKUNDI

Halmashauri ya Lushoto imekuwa ikiwezesha vikundi vya ujasiriamali vya wanawake na vijana kupitia 10% ya mapato ya ndani kwa vikundi tajwa. Kwa maana 5% wanawake na 5% vijana.

3.0 TARATIBU ZA KUFUATA KUOMBA MKOPO KUTOKA MFUKO WA MAENDELEO YA VIJANA NA MFUKO WA MAENDELEO YA WANAWAKE KATIKA HALMASHAURI YA (W) LUSHOTO

3.1 MAHITAJI / VIGEZO ILI KIKUNDI KIWEZE KUPATA MKOPO

- 1) Kikundi cha vijana wa kike au kiume (miaka 15 hadi 35) au kikundi cha wanawake kuanzia miaka 18 na kuendelea. Idadi ya wanakikundi ni watano.
- 2) Wanakikundi wawe ni wakazi wa Halmashauri ya wilaya ya Lushoto
- 3) Wanakikundi wawe na shughuli wanazozifanya zenye uhitaji wa kuongezewa mtaji. Hapa msisitizo zaidi ni kwenye shughuli za kilimo, ufugaji, biashara, usindikaji au viwanda vidogo vidogo.
- 4) Nakala hati ya usajili wa kikundi kutoka Idara ya Maendeleo ya Jamii ya Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto au usajili kutoka kwenye mamlaka zinazotambuliwa kisheria.

- 5) Barua ya kuomba mkopo kwenda kwa Afisa Maendeleo ya Jamii (W) iliyopitishwa na Afisa Mtendaji wa Kata na Afisa Mtendaji wa Kijiji.
- 6) Nakala ya katiba ya kikundi.
- 7) Mchanganuo wa mradi unaoombewa mkopo ukiainisha matumizi, makisio ya mapato tarajiwa, makisio ya faida na kiasi kinachoombwa.
- 8) Muhtasari wa kikao cha wanakikundi kilichopitisha maamuzi ya kuomba mkopo huo wa fedha.
- 9) Namba ya Akaunti ya benki ya kikundi yenye jina la kikundi.

4.0 UTOAJI WA MIKOPO

Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, 2015/2016 na 2016/2017 Halmashauri imetoa mikopo kwa vikundi kwa mchanganuo ufuatao:-

- i. Kutoa mikopo kwa vikundi 13 vya wanawake shilingi milioni ishirini na nne (Tsh 24,000,000/=) kwa mwaka wa fedha 2016/2017, vikundi 7 mwaka wa fedha 2014/2015 Tshs 14,000,000/= na vikundi 5 mwaka wa fedha 2015/2016 Tshs 10,000,000/=
- ii. Vikundi 6 vya vijana vilikopeshwa Tshs 20,000,000/= mwaka wa fedha 2016/2017, vikundi 8 vilikopeshwa Tshs 19,000,000/= mwaka wa fedha 2014/2015 na vikundi 5 vilikopeshwa Tshs 11,000,000/= mwaka wa fedha 2015/2016.

Aidha kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Halmashauri imetenga jumla ya Tshs 148,000,000/= kwa ajili ya kukopesha vikundi vya ujasiriamali vya wanawake na vijana.

5.0 MAFANIKIO

- i. Vikundi 3 vimefanikiwa kupata masoko ya uhakika ya biashara zao. Vikundi hivyo ni Hamasa, Tafakari na Interfaith. Masoko haya ni Serengeti fresh na Homevege ambao wameingia mkataba na wanakikundi wa kununua njegere changa. Soko lingine lililopatikana ni soko la kuku ambapo wanakikundi cha Tafakari wanauza kuku 30 kila wiki.

- ii. Kikundi kingine ni kikundi cha Interfaith ambacho ufyatua matofali ya Interock ambao hupokea tenda za matofali kutoka ndani na nje ya wilaya.
- iii. Vikundi vingine vimefanikiwa kuanzisha mashine za kusaga na kukoboa mahindi kama njia ya kujiongezea kipato na kutengeneza ajira.
- iv. Pia kuna baadhi ya vikundi vimenunua gari na pikipiki kama miradi ya vikundi.
- v. Maisha ya wanawake na vijana walio kwenye vikundi vilivyokopeshwa na Halmashauri yameimalika kwa kiasi kikubwa kutokana na shughuli zao kuongezewa mitaji.

6.0 CHANGAMOTO

- i. Baadhi ya wanavikundi kutokuwa waaminifu katika kufanya marejesho ya mikopo wanayokopa.
- ii. Migogoro ya mara kwa mara katika vikundi ambayo wakati mwingine inahatarisha uhai wa vikundi
- iii. Baadhi ya wanavikundi kutoonyesha ushirikiano katika kufanya kazi kwa pamoja katika miradi ya vikundi

7.0 MIKAKATI YA IDARA

- i. Kuendelea kutoa elimu kwa vikundi ili waweze kuepuka migogoro na waweze kuona umuhimu wa kurejesha mikopo.
- ii. Kuamsha ari ya wanachama wa vikundi kushirikiana katika kufanya shughuli za vikundi kwa pamoja ili kuweza kujiletea maendeleo na hata kufikia kuwekeza katika viwanda vidogovidogo vya kati na vikubwa.
- iii. Kushirikiana na Taasisi wezeshi za kiserikali na zisizo za kiserikali ili kuweza kuwasaidia wanavikundi kuweza kupata mafunzo mbalimbali ya kujikwamua kiuchumi na mikopo.

**Imeandaliwa na Idara ya Maendeleo ya Jamii
Halmashauri ya wilaya Lushoto
22/11/2017**